

Jumuiya Ndogo Ndogo za Kikristu (JNNK) Uzoefu wa Kichungaji wa Tanzania

Na Askofu Method Kilaini

NOTE: This is a talk originally given in Swahili at the Mwanza Metropolitan SCCs Workshop on the theme “Small Christian Communities (SCCs) Embrace the Word of God” at the St. Dominic Pastoral Centre in Mwanza, Tanzania on 20 May, 2014.

I. UTANGULIZI

Ili kuelewa sababu ya mafanikio ya Jumuiya Ndogo Ndogo za Kikristo katika Afrika, kusini mwa jangwa la Sahara, lazima kurudi nyuma na kuona historia yake kitamaduni na kisiasa. Jamii ya Wabantu kimsingi imejengwa juu ya mfumo wa ukoo. Watu wa ukoo mmoja wanajiona ukaribu na kama ukoo ulikuwa mkubwa sana uligawanyika lakini ule wa awali ulibaki kama ukoo mama. Kwa njia hii familia kamwe haikuwa na upweke, bali ilikuwa ni sehemu ya ukoo na ukoo uliipa, hifadhi ya jamii na kulinda maadili ya jamii hiyo. Nje ya ukoo kulikuwa hakuna shughuli ya kijamii.

Baada ya Mtaguso Mkuu wa Pili wa Vatikano, kanisa lilianza kutafuta njia bora ya kuishi kama familia ya Mungu ulivyoagiza mtaguso huo. Kanisa lilijaribu kuiga maisha ya kanisa la mwanzo la mitume huko Yerusalemu. Katika Amerika ya Kusini waliunda ‘Jumuiya za msingi za Kikristo’ Kongo Kinshasa hata kabla ya Mtaguso Mkuu wa Vatikano II, nao walikuwa wanatafuta njia za Kiafrika ya kusihhi iman yao. Katika Afrika ilikuwa ni AMECEA ambayo ilikuja na mpango mkakati madhubuti wa kuunda ‘Jumuiya Ndogo Ndogo za Kikristo’ kama sera ya uinjilishaji.

II. AMECEA NA JUMUIYA NDOGO NDOGO ZA KIKRISTU (JNNK)

Mwanzoni, katika nchi nyingi hata hapa Tanzania, hasa baada ya Mtaguso Mkuu wa Vatikano II, semina na utafiti ulifanywa kutafuta namna ya kuishi maisha ya kanisa kama familia ya Mungu na kuyaweka katika matendo. Kati ya nchi zote za AMECEA, wa kwanza kuchukua hatua madhubuti alikuwa Askofu Patrick Kalilombwe, Mmisionari ya Afrika, akiwa askofu wa Lilongwe Malawi, yeye ulifanya Sinodi ya jimbo ambayo ilianzisha mpango wa kichungaji ukiwa na msingi wake katika Jumuiya Ndogo Ndogo za Kikristu.

Kuanzia Mkutano Mkuu wa AMECEA mwaka 1973 Maaskofu walisisitiza juu ya mpango wa kujikita kwenye JNNK. Mwaka 1976 katika Mkutano mkuu uliofanyika mjini Nairobi, Kenya maaskofu walitangaza rasmi kwamba “*Mkakati mahususi wa kuunda Jumuiya Ndogo Ndogo za Kikristu inabidi upate kipaumbele katika uchungaji nchi ya Afrika ya mashariki*”. Kuanzia hapo JNNK imekuwa ajenda ya kudumu katika mikutano yote ya AMECEA. Mikutano ya miaka 1976, 1979, 1992 na 2002 ilijikita sana juu ya JNNK. Hii ndiyo sababu AMECEA ilipofanya Mkutano Mkuu, Dar es Salaam Tanzania mwaka 2002, mabango yalikuwa yakisomeka “*Karibu AMECEA, mzazi wa jumuiya Ndogo Ndogo za Kikristu*”. Mwaka huo ulikuwa wa 25 tangu JNNK iwe sera rasmi ya AMECEA na kama kumbukumbu ya mkutano huo TEC ilitengeneza vitenge vya Jumuiya Ndogo Ndogo za Kikristu.

III. TANZANIA NA JUMUIYA NDOGO NDOGO ZA KIKRISTU

Rais wa kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alichota katika mfumo wa jadi wa jamii ya Wabatu kuunda mfumo wake wa utawala wa Ujamaa. Kitu kimojawapo alichukua kaya kumi na kuziunda zikawa mashina ya utawala unaojitegemea katika mambo ya msingi. Hii iliongeza ushiriki wa watu katika maamuzi na utawala.

Baadhi ya viongozi wa dini walijiunga na mfumo huu wa Ujamaa. Maarufu kati yao ni askofu Christopher Mwoleka wa jimbo la Rulenge. Hakupokea mfumo huu kinadharia bali alikwenda kuishi katika vijiji vya Ujamaa na kushiriki kikamilifu maisha yao. Kutoka huko alileta wazo la Ujamaa katika kuishi kanisa kama familia ya Mungu, au Jumuiya Ndogo Ndogo za Kikristu. Alikuwa askofu wa kwanza Tanzania kufanya JNNK kama sera ya kichungaji ya jimbo lake. Mwaka 1974 aliweza kwa kijiamini kuwatangazia na kuwahubiri maaskofu juu ya hilo. Aliweza kutengeneza miundo mbinu ya uonogzi katika jumuiya na kuwapa majukumu mbali mbali wanachama katika jumuiya. Sehemu kubwa ya mfumo huo ilichukuliwa na Baraza la Maaskofu katika mwongozo wake wa JNNK.

Baraza la Maaskofu Tanzania walichukua kwa uzito mkubwa maamuzi ya AMECEA ya mwaka 1976 juu ya JNNK. Mwaka 1977 kulikuwa na semina ya kitaifa kuona namna ya kutekeleza uamuzi huo. Waliamua kwamba kipaumbele cha kanisa la Tanzania ni kujenga Jumuiya ndogo ndogo ambazo ni za wanakanisa mahalia, lialoeneza injili kwa kusali pamoja, kusikiliza neno la Mungu, kutiana moyo na kushiriki pamoja katika kutimiza wajibu wao kama wakristu. Jumuiya Ndogo Ndogo ikiwa na msingi wake katika neno la Mungu na Ekaristi Takatifu, inawapa washirika umoja katika imani, matumaini na mapendo (Koinonia); inamshuhudia Bwana Mfufuka na kumtangaza kama Mkombozi (Kerygma), na ulazima wa kutoa huduma (diakonia). Agizo hili lilitekelezwa katika miongozo yote ya kitaifa, kijimbo na katika maparokia.

Nakumbuka nikiwa Katibu Mkuu wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), katika kila mkutano mkuu wa mwaka ilibidi kutoa ripoti juu ya utelelezaji wa JNNK. Karibu katika kila Ujumbe wa Kwaresima, maaskofu waliandika juu ya JNNK. Kwa mfano mwaka 1993, katika barua yao ya "*Dhamira Safi - Dira ya taifa letu*", maaskofu waliomba JNNK zitumike pia kuogeza kipato cha wanajumuiya ili waweze kukidhi mahitaji ya familia. Mwaka 1995 katika barua yao "*Walei wa Tanzania - Mtakuwa Mashahidi Wangu*" (Mdo.1:8) wanasisitiza "*Utume wa Biblia hauna budi kupewa kipaumbele katika uchungaji wa Kanisa. Basi kuweni na Biblia katika familia zenu. Jiwekeeni utaratibu katika maparokia na majimbo wa kupata na kusambaza Maandiko Matakatifu, vitabu vya Sala, Vitabu vya elimu ya dini na magazeti ya Kikristu. Aidha zifanyike semina na mafunzo rahisi kusaidia walei kusoma, kuelewa na kutafakari Neno la Mungu hasa katika jumuiya ndogo ndogo za Kikristu na kila familia. Jijengeeni tabia ya kutafakari Neno la Mungu*". Hata siku za karibuni mwaka 2008 katika barua yao "*Mungu ni Upendo - "Deus Caritas Est"*" (1Yoh 4:16) wanafundisha "*Tukiongozwa na kauli mbiu: "Moyo mmoja na roho moja katika Kristo"*", mwaka huu tunaadhimisha miaka 30 tangu kuasisiwa kwa JNNK. JNNK ni vituo vya upendo; watu wanapaswa kuonja upendo wa Mungu ndani yake. Kielelezo cha JNNK ya kwanza kinapatikana katika kitabu cha Matendo ya Mitume. Kila mtu alijali shida za mwenzake. JNNK zapaswa kuwa vituo vya kushuhudia upendo wa Mungu kwa matendo hai ya kuhusika na kujaliana.

Toka mwanzo wa Kanisa, kujali wasionacho, maskini na wahitaji vimekuwa ndio ishara wazi ya utume wa Kanisa. Utoaji sadaka kwa ajili ya wahitaji ni sehemu muhimu ya wajibu wa

Kanisa (rej. Mdo 2:44; 4:34-37). Kanisa la awali liliweka mashemasi ili wawahudumie wajane na wahitaji (rej. Mdo 6: 1-6). Paulo Mtume aliyaalika makanisa yenye uwezo yachangie kwa ajili ya maskini wa Kanisa la Yerusalemu (rej. 2 Kor 8-9). Ni wakati muafaka, kwa mfano, katika JNNK kuwa na mfuko wa kusaidiana kutatua masuala ya afya, elimu, maafa n.k.”¹

Mkutano Mkuu wa TEC mwaka 1997 waliagiza Tume ya Sheria za Kanisa kurekebisha Katiba ya Halmashauri ya Walei na mwaka 1998 ulipokuwa unaipitisha uliingiza kipengere kwamba viongozi wote wa Halmashauri ya Walei wachaguliwe kuanzia katika JNNK. Haya yalikuwa mapinduzi makubwa sana kwa sababu sasa mtu asingeliweza kuwa kiongozi katika ngazi yo yote bila kuwa na mizizi yake katika JNNK. Hili lilizipa nguvu JNNK na kuimarisha Halmashauri ya Walei katika ngazi zote kuanzia kigango hadi taifa.

Mwaka 2007-2008 ulitangazwa kuwa mwaka wa Jumuiya Ndodo Ndogo za Kikristu. Ulifunguliwa rasmi majimboni siku ya Pentekoste tarehe 27 Mei 2007 na kitaifa wakati wa Mkutano Mkuu wa mwaka tarehe 1 Julai 2007 kwa sadaka takatifu ya misa katika katedrale ya Mtakatifu Yosefu Dar es Salaam.

Jumuiya Ndogo Ndogo za Kikristu zimepewa kipaumbele siyo tu kitaifa bali katika ngazi zote kanisani. Hii inaonyeshwa jinsi sinodi za majimbo mbali mbali katika maazimio yao wanaweka mkazo mkubwa katika kuimarisha JNNK kwa mfano sinodi ya Mwanza, Musoma, Rulenge – Ngara kusema chache zilizokaribu nasi.

IV. UZOEFU WA JUMUIYA NDOGO NDOGO ZA KIKRISTU KATIKA JIMBO KUU LA DSM NA BUKOBA

Nimeishi Dar es Salaam kwa muda wa miaka 20, kumi kama Katibu Mkuu wa Baraza la Maaskofu Tanzania na kumi kata Askofu Msaidizi. Nitaongelea hasa juu ya maika 10 ya jimboni Dar es Salaam na nitaongeza kidogo juu ya jimbo la Bukoba lakini kwa sababu Wanabukoba wapo sitasema sana waje wajisemee.

Katika miaka 10 Jimbo Kuu la Dar es Salaam nilipata uzoefu wa JNNK kwanza kama askofu mwenye jukumu la kutia moyo na kuratibisha na pili kama mwanachama wa kawaida katika mojawapo ya jumuiya. Nilifurahia zaidi hii ya pili.

a. JUMUIYA NDOGO NDOGO ZA KIKRISTU KAMA ASKOFU

Jijini Dar es Salaam kama Bukoba, JNNK ni nguzo ya uinjilishaji na kazi zote za uchungaji. Kupata huduma za kiroho parokiani huanzia katika JNNK, ni viongozi wa jumuiya wanaoorodhesha wagonjwa ili wapate huduma ya kiroho, watoto na vijana wa kupata mafundisho ya dini kwa ajili ya kupata sakramenti nk. Fomu zinajazwa na kutiwa sahihi na viongozi hao kuthibitisha ustahilivu wa kupata huduma husika. Wao ndio mlango wa shughuli za kikanisa kwa waamini.

¹ Ujumbe wa Kwaresima 2008 “Mungu Ni Upendo - “*Deus Caritas Est*” (1Yoh 4:16) No. 5.3 Upendo wa Mungu katika Jumuiya Ndogo Ndogo za Kikristo.

Mwaka 2006 – 2007 Jimbo Kuu la Dar es Salaam lilitangaza mwaka wa “Jumuiya Ndogo Ndogo za Kikristu”. Mwaka ulifunguliwa siku ya somo wa Jimbo Kuu, Makatifu Yosefu, tarehe 20 Machi na kwa kutoa alama ya kukumbuka maparoko walionjeshwa chumvi ili wawe chumvi katika JNNK na wenyeviti wa JNNK waliwasha mishumaa yao kutoka mshumaa wa Pasaka. Mwaka uliotangulia wanaume wote, katika hija yao Pugu, walikuwa wameonjeshwa chumvi. Ishara hii ni kuwapa kumbukumbu inayoonekana na kukumbukwa. Katika mwaka huo kanisa lilitafakari mafanikio na mapungufu katika utekelezaji wa mfumo huo wa uchungaji. Vile vile lilitumia fursa hiyo kupanga namna ya kusonga mbele. Fursa hiyo ilitumiwa kusheherekea na kuhamasisha JNNK kupitia semina, maadhimisho ya ibada, maandamano, hija, vipindi redioni na nyimbo kuhamasisha JNNK. Salamu ya mwaka huo ilikuwa “*Jumuiya Ndogo Ndogo za Kikristu*” jibu “*Chombo cha Uinjilishaji*”. Mwaka ulikuwa na mafanikio makubwa. Somo ni kwamba tufanye juhudi watu wasibweteke bali tubuni njia mbali za kuwapa nguvu.

Kama Askofu licha ya mimi binafsi kupenda sana JNNK nilishika jukumu langu la kutembelea na kuwapa moyo jumuiya mbali mbali. Kusema ukweli nilipenda sanakutembelea JNNK hata huku Bukoba. Inapendeza kukutana na watu katika mazingira yao manyumbani mwao na kuwaona kama wanavyoishi kikawaida. Kuwa pamoja nao katika furaha na katika shida. Hata unapooonea nao wako kawaida bila woga au heshima zisizo za lazima. Mwishowe unaona kwamba inakuwa kama sehemu ya kupumzika. Wote walijua kwamba napenda kwenda katika jumuiya hivyo walinalika mara nyingi. Hilo liliwapa nao fursa ya kukutana, kupanga na kuwapa shughuli za pamoja. JNNK bila mambo ya kufanya pamoja na kujibiidisha pamoja inaduwaa.

Hata Bukoba ni hivyo hivyo ila mipango inakuwa tofauti. Bukoba askofu hutembelea rasmi kila parokia mara moja katika miaka miwili. Hukaa parokiani kwa siku tatu hadi nne ili kukutana na watu mbali mbali na kufanya ukaguzi. Katika kila parokia, licha ya Jumapili kuwa siku ya kutoa kipaimara, natenga siku moja kwa ajili ya kutembelea jumuiya mojawapo. Tunaadhimisha pamoja ibada ya misa na siku hiyo unakaa nao na kusikiliza furaha, shida na mategemeo yao. Katika sehemu zote mbili DSM na Bukoba hali ni ile ile, furahi na ushiriki wa hali ya juu.

b. UZOEFU KAMA MWANAJUMUIYA

Nilipoteuliwa kuwa askofu msaidizi wa Jimbo Kuu la DSM, nilipewa nyumba ya zamani ya ubalozi wa Vatikano ambayo iko katika sehemu iliyotengwa ya matajiri, Masaki- Oysterbay. Kwa sababu sikufanyia ofisi huko hivyo majirani hakuna aliyekuja hapo. Masaki kila mmoja nyumba yake imezungukiwa ukuta tangazo la kuna mbwa wakali, walinzi wa sekuliti au mataa ya kumulika wezi nk. Kule huwezi kuingia nyumba ya mtu mpaka uwe umealikwa rasmi. Nilipoamua kujiunga na JNNK ya Bikira Maria Mpalizwa pale mambo yaligeuka. Milango yetu ikafunguliwa nasi tukawa na zamu ya watu kusali kwetu. Vile vile na nyumba za majirani zetu zikafunguliwa tukienda huko nyumba kwa nyumba kusali. Majirani zetu walikuwa kutoka kwa mawaziri, majaji wa mahakama kuu na ya rufaa, wanyabiashara wakubwa na wakurugenzi lakini vile vile wasichana watumishi wa nyumbani, mama ntilie, wauza viosk na walinzi. Katika jumuiya nilikuwa kama mwanajumuiya mwingine ila mwishoni niliwapa Baraka au kama ilihitajika ibada ya kikuhani. Kusema kweli mtu ulingojea kwa hamu siku ya jumuyia ambayo ilikuwa Jumatano jioni.

Jumuiya yetu ilishamiri na wanaume wakaudhuria kwa wingi hata kuliko wanawake. Wengine wakasema kwa sababu kuna askofu mwanamume mwenzao. Jumuiya za karibu zikaomba nazo nizitembelee hivyo tutafanya umoja wa jumuiya za Masaki ambazo tulikutana mara moja kwa mwezi.

Maisha ya jiji na magumu na kuna watu kutoka lika, jamii na kabila mbali mbali. Hali ya kiuchumi na kijamii inatofautiana, kuna matajiri wa kutupwa na maskini walala hoi, wenye nyumba kama ilulu na wanaolala barabarani, wanafamilia na Makahaba, watakatifu na wahuni, wasomi na wasiujua kuandika. Uijilishaji jijini ni kuwaleta pamoja lika zote hizo na kuunda kanisa moja kama familia ya Mungu. Kijijini utofauti wa watu siyo mkubwa kiasi hicho lakini shida ni hiyo hiyo.

Mtu akiya mjini hajulikani na mara nyingine hajiheshimu kwa sababu anakuwa mpweke. Haoni haya ni kama mtu bila jina au ukoo. Hata pale Masaki ambapo palionekana tajiri lakini matajiri hao walijifungia na shida zao. JNNK zinampa mtu ukoo, zinampa jina kiasi kwamba majirani wanafahamiana na kuitana kwa majina. Watu ambao wameacha jamii na ndugu zao na sasa wanaelea wanapewa kishikizo, wanapata jumuiya ambako wanasaidiana katika kujenga na kuendeleza wema. Kristo anakuwa kiungo chao.

Jumuiya ndogo ndogo zimekuwa mkombozi. Watu wanafahamiana, wanasalimiana, wanasali pamoja na kuweza kupaga pamoja. Kule Masaki ilipendeza kumwona mama Ntilie akiingia bila woga kwa nyumba ya waziri au jaji wa mahakama ya rufaa na kuanza kuongea nao. Katika umoja wa jumuiya tulikuwa hata na mke wa waziri mkuu, Regina Lowasa, ilipendeza kuona licha ya kwamba ana body guard watu wanaweza kusuguana bega naye na kutaniana. Naye alijisikia kujiachia. Watoto ni wazuri hawana ubaguzi hivyo unaona wote wanacheza na kukimbia pamoja na kutembeleana bila kujali hadhi ya wazazi wao. Watoto wengine kupitia urafiki huo wanasaidiwa.

V. KWA NINI TUWE NA JUMUIYA NDOGO NDOGO

a. JNNK Zinajenga Ujirani Mwema

Jumuiya Ndodo Ndogo za Kikristu hasa katika miji zimejenga ujirani wa watu wanaofahamiana na kuhusiana. Kwa sababu mikutano inafanyika kwa kuzunguka nyumba hadi nyumba ukaribu unakuwa mkubwa zaidi kwa sababu mtu anakuwa siyo tu na sura, bali anakuwa jirani unayemfahanu na kufahamu familia yake. Pole pole wanakuwa marafiki na kushirikishana katika furaha na katika majonzi na shida. Tukiwa pale Masaki tuliweza kuunda vikundi vya vijana, wanawake na watoto.

b. Jumuiya Ndogo Ndogo kama Chombo cha Uinjilishaji

Dar es Salaam parokia nyingi zilijengwa na JNNK. Watu walipohamia katika sehemu mpya wengi wao Jumapili walirudi katika parokia walikotoka kwa sababu rafiki zao walikuwa huko. Lakini kadiri siku zilivyokwenda waamini shupavu wachache walikuja pamoja na kuunda JNNK na kuanza kusali pamoja. Pole pole mtu alitoa sehemu ya ardhi yake na walijenga kibanda cha kusalia ambacho walivyoongezeka kilipanuliwa na mwishowe walinunua ardhi na kujenga kigango ambacho mwishowe kilikuwa parokia. Kupitia JNNK wakristu wenyewe kwa wenyewe walihamasishana na kupeana nguvu. Hivyo hivyo ni

wanajumuiya hao ambao walitembelea wahamiaji wapya na kuwaigiza katika ushirika wa jumuiya zao. Kwa namna hiyo JNNK zimekuwa taasisi za kimisionari. Hata vijinini JNNK zinasaidia sana kuwatafuta waamini waliolegea.

c. Jumuiya Ndogo Ndogo kama mhimili wa Maisha ya Kikristu

Jumuiya zinaboresha sana maisha ya kiroho ya waamini iwe ni mjini au kijijini. Kwanza waamini wana ushirika wa kuhimizana kufanya mema. Mtu anajisikia asiwaangushe wenzake kwa maisha mabaya. Mtu ana jina lake kama Mkristu analoona lazima kulinda hadhi yake. Anajiona mwenza wa wengine, anaingia nyumba zao nao wanaingia ya kwake hata kama ni maskini. Jumuiya ni kama SACCOS ya maadili mazuri na wema. JNNK inampa mtu heshima na hadhi.

JNNK inamtoa mtu katika upweke. Anapata watu ambao anaweza kuongea nao mambo mbali mbali yakiwemo yale yanayompa shida. Kiurahisi atapa mtu wa kuweza kumpa ushauri katika maisha yake. Pamakuwepo na mshikamano katika raha na shida, matukio kama ndoa au kifo na mengine ya maisha.

Watoto wakijuana inaleta amani kwa wazazi kwa sababu hawaogopi mtoto wao amepokwenda jirani atajifunza nini huko. Wazazi wanaweza kupanga pamoja namna ya kulea watoto wao. Shule nyingi za chekechea zimeanzishwa hivyo.

Vijana wanakuja pamoja na kushirikiana katika vyama na hata kupata wachumba kupitia katika uhusiano wa jumuiya. Wanawake na wanaume vile vile wanaimalika kiroho na katika kuunda vikundi katika jumuiya. Kwa namna hiyo JNNK inakuwa familia ya Mungu.

d. Jumuiya Ndogo Ndogo na Miundo Mbinu ya Kanisa

JNNK inakuwa ndiyo taasisi ya msingi baada ya familia katika miundo mbinu ya kanisa AMECEA. Jumuiya zimerahisisha uongozi na mawasiliano katika parokia. Shughuli zote za parokia huanzia katika JNNK iwe ni sakramenti au uchaguzi wa viongozi. Hata na uchangishaji wa pesa kwa ajili ya maendeleo ya jumuiya, kigango, parokia au kanisa hufanikishwa na JNNK. Jumuiya hurahisisha ushirikishwaji kwamba mawazo kutoka kwa watu kupitia JNNK kwenda kwa uongozi wa juu na vile vile mawazo kutoka juu huwafikia watu kupitia JNNK.

e. Jumuiya Ndogo Ndogo na madhehebu na dini nyingine

Jumuiya Ndogo Ndogo zimesaidia kuleta mahusiano mazuri na madhehebu ya dini nyingine. Mara nyingi watu wanaoishi pamoja waliwasiliana kwa namna mbali mbali hata kuunda vyama vya kusaidiana lakini katika ngazi za dini walijiona hawana cha kushirikishana. JNNK zimeweza kuleta mahusiano hayo kwa sababu Jumuiya Ndogo Ndogo za Kikristu kawaida huwaalika waamini wa madhehebu mengine wanapokuwa wanasheherekea matukio katika jumuiya. Hilo huleta uhusiano hata katika nyanja za kidini, mitaani na vijijini na kuondoa kubaguana na kusengenyana kidini. Zimwi likujualo halikuli likakwisha. Kupitia JNNK wanajuana na kubadilishana mawazona misaada. Siku moja askofu mmoja wa Kiluteri aliniomba nimweleze JNNK zinaendeshwaje ili naye azianzishe.

VI. CHANGAMOTO NILIZOZIONA KATIKA KUENDESHA JNNK

- a. Sharti la kwanza la mafanikio ya JNNK ni upendo, ushiriki na usimamizi mzuri wa paroko na mapadre wenzake. Huwezi kushauri utamu wa kitu kama wewe huonji. Mara nyingine mapadre wanatoa ushauri wa mdomo lakini hawaonyeshi kwa matendo.
- b. Wanaume ingawa wengi wanaunga mkono na wako tayari kuchangia kifedha na mali kutimiliza malengo ya JNNK, hawashiriki katika mikutano ya kila wiki bali kuonekana katika matokeo makubwa na sikukuu.
- c. Mjini kuhamahama kwa watu hasa kama kunahusisha viongozi huathili maendeleo ya jumuiya.
- d. Jumuiya nyingine zimekuwa kubwa mno lakini wanachama hawataki kuzivunja shauri ya kuzoeana, hilo linatatiza uendeshaji mzuri wa jumuiya. Mahali pengine baada ya kugawa jumuiya wanakuwa na jumuiya mama na mara nyingi ndiyo inafanya kazi.
- e. Mjini wanajumuiya wengine wanapata shida kuwaalika wenzao katika nyumba za kupanga kwa sababu mwenye nyumba hataki.
- f. Jumuiya bado hazijaanza kuongea na kutenda juu ya shida za kijamii hasa zile za haki na amani. JNNK zinaganga vidonda lakini haziulizi kwa nini kuna vidonda, zinaganga njaa lakini hazikabiliani na sababu ya njaa.
- g. Kwa kuogopa kuingilia siasa JNNK haziwatii moyo watu wazuri kugombea nafasi za utawala kisiasa na kijamii.

VII. TAMATI

Mafaniko ya kanisa mbeleni yanategemea kwa sehemu kubwa mafanikio ya Jumuiya Ndogo Ndogo za Kikristu. Miaka michache iliyopita nilikuwa kusini mwa India. Nilishangaa kuonana wenyewe wanaanza kufuata mfumo wa Jumuiya Ndogo Ndogo wakiwa na mikakati kama ya kwetu. Wao wanaziita 'Jumuiya za Msingi za Kikristu'. Jumuiya zao ni changa zina umri usiofikia miaka 20 lakini hilo linaonyesha kwamba sera ya JNNK kama mfumo wa uinjilishaji unakuwa wa kimataifa. Tunaishukuru AMECEA mzazi wa Jumuiya Ndogo Ndogo za Kikristu ambao wanendelea kuchochea Baraka hiyo. Tunamshukuru Mwanajumuiya Padre Joseph Healey, MM ambaye tangu enzi za askofu Christopher Mwoleka amekuwa taa isiyozimika ya kuendeleza Jumuiya Ndogo Ndogo za Kikristu.

Tanzania Bishop Method Kilaini is the Auxiliary Bishop of Bukoba Diocese, Tanzania. He is a Church Historian.

Email: mkilaini@gmail.com